Ulizia Njia Za Zamani

(Ask For The Old Paths)

Na

Ellis P. Forsman

Ulizia Njia Za Zamani

(Ask For The Old Paths)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Ulizia Njia Za Zamani

Yer. 6:16

Agano la Kale limejawa na masomo mengi kwa ajili ya Wakristo.

Iliandikwa kwa ajili ya kujifunza kwetu – Rum. 15:4, "*Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini.*"

Yaliandikwa kwa ajili ya kutuonya – 1 Kor. 10:11, "*Basi mambo hayo yaliwapata wao kwa jinsi ya mifano yakaandikwa ili kutuonya sisi, sisi tuliyofikiliwa na miisho ya zamani.*"

Moja ya somo hilo ni ile inayopatikana katika siku za Yeremia. Huu ulikuwa ni wakati wa dini na dhiki ya kijamii. Taifa la Israeli lilikuwa likipelekwa katika kila mwelekeo.

Bwana alitaka kuwapa pumziko la nafsi zao. Yer. 6:16, "*BWANA asema hivi simameni katika njia kuu, mkaone , mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipaatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema hatutaki kwenda katika njia hiyo.*"

Akitumia taswira ya wasafiri waliopotea njia, Bwana anawaita ku…

Kuuliza Njia Za Zamani

Bwana anafanya ombi lake katika musitari huu. Yer. 6:16, "BWANA asema hivi simameni katika njia kuu, mkaone , mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mtajipaatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema hatutaki kwenda katika njia hiyo."

Hakuna njia moja pekee. Kuna njia nyingi mtu anaweza kufuata.

"*Mkaulize habari za mapito ya zamani*". (Yer. 6:16, hapo juu). 'Njia ya zamani' siku zote ni njia nzuri. Yawezekana hili ndio swala hapa. "*I wapi njia iliyo njema*?" (Yer. 6:16). Kuna njia nyingi ambazo wanadamu wanafuata, lakini sio njia nyingi zinazoongoza katika 'njia nzuri'.

Katika swala hili, njia ya zamani iliongoza zamani katika Sheria ya Musa. Yer. 7:22-24, "*Maana sikusema na baba zenu, wala sikuwaamuru kwa habari ya sadaka za kuteketeza na dhabihu, siku ile nilipowatoa katika nchi ya Misri; lakini naliwaaamuru neno hili nikisema, sikilizeni sauti yangu nami nitakuwa Mungu wenu nanyi mtakuwa watu wangu; mkaende katika njia ile yote nitakayowaamuru mpate kufanikiwa. Lakini hawakusikiliza , wala kutega sikio lao, bali walikwenda kwa mashauri*

yao wenyewe na kwa ushupavu wa mioyo yao mibaya, wakaenda nyuma wala si mbele."

Yesu pia anawasihi vivyo hivyo leo; kujitahidi kutembea kaatika njia sahihi. Luka 13:24, "*Jitahidini kuingia katika mlango ulio mwembamba , kwa maana nawaambia ya kwamba wengi watataka kuingia, wasiweze.*"

Njia hii ina mlango mwembamba, na haipiti kirahisi; ambapo kuna njia moja tu kwenda kwa Baba. Yoh. 14:6, "*Yesu akamwambia, mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi.*" Mdo. 4:12, "*Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"

Maana kuna njia nyingine pana, ambazo mtu anaweza kufuata. Mat. 7:13, "*Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo.*"

Hii ndio njia ambayo wengi hufuata; hii ndio njia inayoelekea upotevuni.

Wakati njia ambayo Yesu anatoa ni 'njia nzuri'; ambapo pia anatoa pumziko la nafsi. Mat. 11:28, "*Njooni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.*"

Katika shauri hili, njia ianaongoza kurudi katika maneno ya Yesu. Mat. 11:29, "*Jitieni nira yangu mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu.*"

Maneno ya Yesu hufanana "zamani" na viwango vya leo. Kilichowatokea Waisraeli inaonekana kuwa tatizo la wengi leo. Kama ilivyoelezwa katika Yer. 18:15, walikuwa wamejikwaa. Yer. 18:15, "*Maana watu wangu wamenisahau, wameufukuzia ubatili uvumba; nao wamewakaza katika njia zao, katika mapito ya zamani, ili wapite katika njia za kando, katika njia isiyotengenezwa.*"

Kutoka Katika Njia Za Wazee, Kutembea Katika Njia

Israeli ilijikwaa. Kwa nini? Kwa sababu walimsahau Mungu. Yer. 18:15, "*Maana watu wangu wamenisahau, wameufukuzia ubatili uvumba; nao wamewakaza katika njia zao, katika mapito ya zamani, ili wapite katika njia za kando, katika njia isiyotengenezwa.*"

Hata kama Mungu alijidhihirisha mwenyewe na mapenzi yake zaamani za kale. Alianzisha "njia" kwa wao kufuata. Badala yake, walizigeukia zingine za pembeni "njia".

Leo watu wa Mungu hukumbana na hatari kama hiyo.

Yesu alianzisha “njia” ili tufuate:

Kwa maneno yake, fundisho, na maagizo. Mat. 11:29, “*Jitioeni nira yangu mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu.*”

Aliwasiliana kupitia mitume wake. Mat. 28:20, “*Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukaamilifu wa dahari.*”

Walipokuwa wakisaidiwa na Roho Mtakatifu. Yoh. 16:12-13, “*Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayosikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.*”

Ambayo wanafunzi wa kwanza walikuwa makini katika kuifuata. Mdo. 2:42, “*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.*”

Ambayo Wakristo wameagizwa kuifuata. 2 Thes. 2:15, “*Basi ndugu simameni imara mkayashike mapokeo mliofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu.” 2 Thes. 3:6, “Ndugu twawaagiza katika jina la Bwana Yesu Kristo, jitengeni nafsi zenu na kila ndugu aendaye bila utaratibu, wala si kwa kufuata mapokeo mliyoyapokea kwetu.*”

Alafu bado kuna “njia” ya mwanadamu inayoweza kutupotosha.

Kama mafundisho ya wanadamu. Mat. 15:9, “*Nao waniabudu bure wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*”

Kama filosofia ya wanadamu. Kol. 2:8, “*Tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba.*”

Mara nyingi imefungashwa kama “mpya!” na “kuendelezwa!” mafundisho kama hayo na Filosofia zinashindwa kutoa kile tu ambacho Bwana anatoa (“inaachwa kwa ajili ya nafsi yako”). Kuhakikisha kwamba hatupotoshwi, tunapaswa ku…

Weka Alama Za Njia, Tengeneza Miti Ikuongoze

Hii ilikuwa ndio suluhisho kwa Israeli; kuweka alama za barabarani ambazo zingewaongoza kurudi katika njia sahihi. Yer. 31:21, “*Jiwekee alama za njia, jifanyie miti ya kukuongoza; uuelekeze moyo wako kwenye njia kuu, njia ile ile uliyoiendea; rudi tena, ee bikira wa Israeli, irudie hii miji yako.*”

Kwa wao, hii "mabando" na "mipaka" ilikuwa ni Sheria ya Musa; ambazo hawakutakiwa kuzidisha au kupunguza. Kumb. 4:1-2, "*Na sasa, Ee Israeli zilikilizeni amri na hukumu niwafundishazo ili mzitende mpate kuishi na kuingia na kuimiliki nchi awapayo BWANA Mungu wa baba zenu. Msiliongeze neno niwaamrulo wala msilipunguze, mpate kuzishika amri za BWANA Mungu wenu niwaamuruzo.*"

Walipaswa kufundisha hili kila kizazi. Kumb. 4:9, "*Lakini jihadhari nafsi yako, ukailinde roho yako kwa bidii usije ukayasahau mambo yale uliyoyaona kwa macho yako, yakaondoka moyoni mwako siku zote za maisha yako; bali uwajulishe watoto wako na watoto wa watoto wako;*"

Hili ndio suluhisho kwetu sisi leo: kuweka alama za barabarani ambazo zitatuongoza katika njia sahihi.

Kwetu sisi, "mabango" haya na "alama hizi" zinapatikana katika mafundisho ya mitume, ambayo ni neno la Mungu.

- Mdo. 2:42, "*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.*"
- 1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*"
- 1 Thes. 2:13, "*Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa, mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo ilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini.*"

Maana zinamafundisho ya Kristo, bila hivyo hatuwezi kuwa na Mungu. 2 Yoh. 1:9, "*Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.*"

Hitimisho

Je unapenda kuwa na pumziko la nafsi yako? Uhuru kutoka dhambini; uhuru kutoka katika makosa? Kwa amani ya ndani na utulivu miongoni mwa adhabu ya nje?

Njia inayoongoza katika pumziko hilo ni njia za zamani zinazopatikana tu kwake ambaye aliishi na kufa kwa ajili ya dhambi zetu karibia miaka 2000 iliyopita; ambaye mafundisho yake yametunzwa kwa uaminifu na mitume wake katika Agano Jipya.

Kama unajikwaa katika maisha, basi "Ulizia Njia Za Zamani" ambazo zitakuongoza umrudie Mungu!

Mtu anafanyikaje Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhim zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb.11:6, "*Maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana yeye ajye kwa Mungu lazima aamini kwamba yeye ndiye, na kwamba huwapa dhawabu wale wote wamtafutao.*" Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17) kijana mmoja jirani yangu miaka sawa na ya kwangu aliniambia kuwa aamini katika Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nikachukua muda wa kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ilikuwa nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamab kuna Mungu. Lakini ilikuwa sehemu yenye usalama, niheri aende kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) katika siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda Mungu atamuruhusu aingie mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Matend 11:18, "*...Mungu amewajalia hata mataifa nao toba <u>iletayo uzima.</u>*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, ukafikiria mwenyewe, "kuna mwizi humu ndani!" Na unachukua simu yako na kuwa pigia polisi, ukiwambia kuwa kuna mwizi nyumbani kwako. Muda mfupi unasikia wanafika na kumshika mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi lazima aombe msaha kwamba hataiba tena na kubadilisha maisha yake. Ni badiliko la nia linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kufanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana <u>kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu</u>.*" Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba kifungu hicho kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "Katika"

inamaanisha kuelekea kitu Fulani; siyo kwamba tayari amesha pata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote, "Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa. Kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akambatiza. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye." (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema "imekuwa kwetu sisi "kuitimiza haki yote" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

  Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Matend. 2:38). Petro, umesema ni nini maana ya ubatizo? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi.*" Kwa nini yeyote anaweza kuacha hatua inayotuondoa dhambi?

  Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tuzikwe. "*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

  Anania alimwambia Paulo (kabla hajaitwa Paulo) kitu kile kile "*Sasa unakaawilia nini? Simama, na ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana.*" (Matend. 22:16).

  Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

  Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Waru 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena.*" (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani yake Mungu kwa kupaka damu yake Kristo katika maisha yetu kwa

ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi “kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuziki mwili kaburini kwa kuweka udongo mdogo juu yake; tunazika mwili.

Kama hujawa Mkristo, kwa nini usizingatie leo?